**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA KWA AJILI YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA WA MWAKA 2024 ULIOFANYIKA KWA SIKU 10 (TEREHE 11 HADI 20 OKTOBA, 2024)

**Ndugu Wanahabari,** napenda niwapongeze kwa mara nyingine tena kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya katika kipindi hiki chote cha uandikishaji tangu tulipozindua rasmi uandikishaji siku ya tarehe 11 Oktoba, 2024 pale katika Kijiji cha Chamwino, Kitongoji cha Sokoine mpaka sasa ambapo tumehitimisha zoezi la uandikishaji. Kwa namna ya pekee mmefanya kazi kubwa sana sana ya kuhabarisha umma juu ya jambo hili na umma umeelewa na kujitokeza kujiandikisha na kwa pamoja tumefanikisha zoezi hili.

**Ndgu Wanahabari,** Uandikishaji wa wapiga kura wa uchaguzi wa wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji pamoja na wajumbe wa Halmashauri ya kijiji na Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umefanyika kwa muda wa siku 10 kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2024 na kuhitimishwa tarehe 20 Oktoba, 2024. Zoezi hilo limefanyika kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2024, Tangazo la Serikali Na. 571, 572, 573 na 574 yote ya tarehe 12 Julai, 2024.

Kanuni hizo zinaelekeza kuwa kutakuwa na orodha ya wapiga kura ambayo itatumika katika uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa mtaa, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa serikali za vijiji na kamati za mitaa.

**Ndugu Wanahabari,** nifuraha yangu kukutana nanyi leo ili kuwapa taarifa rasmi watanzania kuhusu kuhitimishwa kwa zoezi la uandikishaji na matokeo ya zoezi hilo. Muhtasari wa matokeo ya uandikishaji ni kama ifuatavyo:-

1. Jumla ya wapiga kura **31,282,331** wamejiandikisha kupiga kura sawa na asilimia **94.83** ya lengo la kuandikisha watu **32,987,579** ambapo wanaume ni **15,236,772** sawa na asilimia **48.71** na wanawake ni **16,045,559** sawa na asilimia **51.29**.

2. Mwenendo wa uandikishaji kwa kila siku kwa kipindi cha siku 10 ulikadiriwa kuandikisha wastani wa asilimia 10 kwa siku ili kufikia lengo lililokusudiwa. Aidha,mwenendo wa uandikishaji halisi ulikuwa kama ifuatavyo:-

    (i) Siku ya kwanza waliandikishwa watu 3,882,994 sawa na asilimia 11.82 ya lengo la siku la kuandikisha kwa asilimia 10,
    (ii) Siku ya pili waliandikishwa watu 2,554,375 sawa na asilimia 7.78 ya lengo la siku,
    (iii) Siku ya tatu waliandikishwa watu 2,660,084 sawa na asilimia 8.10,
    (iv) Siku ya nne waliandikishwa watu 2,544,844 sawa na asilimia 7.75,
    (v) Siku ya tano waliandikishwa watu 2,460,664 sawa na asilimia 7.46,
    (vi) Siku ya sita waliandikishwa watu 2,472,605 sawa na asilimia 7.50
    (vii) Siku ya saba waliandikishwa watu 2,971,219 sawa na asilimia 9.01,
    (viii) Siku ya nane waliandikishwa watu 3,409,211 sawa na asilimia 10.33,
    (ix) Siku ya tisa waliandikishwa watu 3,813,999 sawa na asilimia 11.56 na
    (x) Siku ya kumi waliandikishwa watu 4,512,336 sawa na asilimia 13.68 ya lengo la siku.

**Ndugu Wanahabari, m**atokeo ya jumla ya uandikishaji kwa kila Mkoa ni kama ifuatavyo:-

| NA. | MKOA | MAKADIRIO YA WAPIGA KURA | WAPIGA KURA WALIOJIANDIKISHA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pwani | 1,224,666.00 | 1,379,079.00 | 112.61 |
| 2 | Tanga | 1,464,618.00 | 1,623,118.00 | 110.82 |
| 3 | Mwanza | 1,954,443.00 | 2,082,973.00 | 106.58 |
| 4 | Dodoma | 1,712,472.00 | 1,784,260.00 | 104.19 |
| 5 | Iringa | 700,833.00 | 704,634.00 | 100.54 |
| 6 | Morogoro | 1,857,302.00 | 1,806,190.00 | 97.25 |
| 7 | Songwe | 716,510.00 | 696,746.00 | 97.24 |
| 8 | Kagera | 1,566,530.00 | 1,522,919.00 | 97.22 |
| 9 | Kigoma | 1,211,122.00 | 1,175,027.00 | 97.02 |
| 10 | DSM | 3,599,247.00 | 3,483,970.00 | 96.80 |
| 11 | Shinyanga | 1,158,025.00 | 1,105,443.00 | 95.46 |
| 12 | Mbeya | 1,352,125.00 | 1,274,565.00 | 94.26 |
| 13 | Arusha | 1,335,884.00 | 1,248,266.00 | 93.44 |
| 14 | Kilimanjaro | 1,172,394.00 | 1,090,312.00 | 93.00 |
| 15 | Singida | 1,022,356.00 | 946,467.00 | 92.58 |
| 16 | Geita | 1,448,821.00 | 1,338,157.00 | 92.36 |
| 17 | Ruvuma | 1,071,231.00 | 989,241.00 | 92.35 |
| 18 | Manyara | 991,317.00 | 895,696.00 | 90.35 |
| 19 | Lindi | 744,442.00 | 648,076.00 | 87.06 |
| 20 | Tabora | 1,652,564.00 | 1,431,874.00 | 86.65 |
| 21 | Njombe | 532,067.00 | 457,317.00 | 85.95 |
| 22 | Katavi | 553,284.00 | 473,724.00 | 85.62 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 23 | Mtwara | 1,025,220.00 | 862,374.00 | 84.12 |
| 24 | Mara | 1,178,695.00 | 965,860.00 | 81.94 |
| 25 | Simiyu | 996,633.00 | 815,056.00 | 81.78 |
| 26 | Rukwa | 744,778.00 | 480,987.00 | 64.58 |
| | **JUMLA** | **32,987,579.00** | **31,282,331.00** | **94.83** |

**Ndugu Wanahabari,** kwa ujumla mikoa yote 26 imefanya kazi nzuri katika zoezi hili la uandikishaji. Matokeo haya yanaonesha kumekuwa na ongezeko kubwa la idadi ya wananchi waliojitokeza kujiandikisha ikilinganishwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 ambapo waliandikishwa wapiga kura **19,681,259** sawa na **asilimia 86** ya lengo lililokuwa limewekwa la kuandikisha wapiga kura **22,916,412**. Mafanikio haya yamechangiwa na uwekezaji mkubwa wa uelimishaji na uhamasishaji katika ngazi zote za muhimu ikiwemo Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Ndugu Wanahabari,** kufuatia matokeo hayo mazuri ya uandikishaji, nichukue fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Watanzania wote waliojitokeza kujiandikisha kwa kuwa tayari wamepata sifa ya kisheria ya kutekeleza haki yao ya kikatiba ya kuchaguliwa na kuchagua Viongozi wa Serikali za Mitaa wanaowataka ifikapo tarehe 27 Novemba, 2024 siku ya kupiga kura.

Aidha, niwashukuru wadau mbalimbali wakiwemo vyombo vya habari, Viongozi wa dini,Viongozi wa kimila, Tasasi za kiraia, wasanii, vyama vya siasa na wadau wengine kwa kuwahamasisha na kuwaelimisha watanzania wenye sifa kujitokeza kwa wingi katika kujiandikisha.

**Ndugu Wanahabari,** baada ya kukamilishwa kwa zoezi la uandikishaji, orodha ya wapiga kura inabandikwa kuanzia leo katika sehemu za matangazo ya uchaguzi kwenye vijiji na mitaa ili kuwezesha wananchi wakague orodha hiyo ili kuomba aidha kurekebisha majina, kubadilisha taarifa zilizoko katika orodha hiyo au kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki.

Ukaguzi huo utafanyika kwa muda wa siku 7 kuanzia leo tarehe 21 - 27 Oktoba, 2024. Hivyo, wananchi wote waliojiandikisha ni muhimu mkajitokeza kuhakiki orodha hiyo.

**Ndugu Wanahabari,** napenda kutoa rai kwa wananchi wenye sifa za kuchaguliwa kuwa viongozi wajitokeze kuanzia **tarehe 26 Oktoba hadi tarehe 1 Novemba, 2024** ili waweze kutimiza haki yao ya kikatiba ya kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi huu.

Zoezi la kuchukua na kurudisha fomu litafanyika ndani ya siku saba (7) kwa tarehe nilizozitaja. Niwasisitize vyama vya siasa kuhamasisha wanachama wao kujitokeza na kugombea nafasi mbalimbali za uongozi ili wananchi waweze kuwa na uwanja mpana wa kuchagua viongozi bora watakaowaletea maendeleo kwenye maeneo yao.

Niendelee kuvishukuru vyama vya siasa kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kutupatia katika zoezi hili, nitoe rai vyama vyote vya siasa viendelee kuwasihi wanachama wao kuendelea kudumisha amani na utulivu. Niwasihi wananchi wa vyama vyote kufuata sheria, kanuni na miongozo ya uchaguzi husika ili kulinda amani, utulivu na ustawi wa nchi yetu.

**Ndugu Wanahabari,** naendelea kuviomba vyombo vya dola kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu tunapoendelea na mchakato huu ili Wananchi wote waweze kushiriki uchaguzi huu kwa amani na utulivu.

Mwisho niendelee kuwasisitiza wasimamizi wa uchaguzi na wadau wote wa uchaguzi kuendelea kuzingatia Sheria na Kanuni za Uchaguzi ili kuhakikisha kuwa uchaguzi huu unaendelea kuendeshwa kwa misingi ya Sheria na Kanuni zilizowekwa, kuwa huru na wa haki na wananchi wote wenye sifa waweze kushiriki. Wakati wa zoezi la uchukuaji na urejeshaji wa fomu hakikisheni wagombea wote wanahudumiwa kwa wakati pasipokuwepo na changamoto zozote. Hakikisheni vyama vyote vimepata maelekezo sahihi kuhusu uchukuaji na urejeshaji wa fomu pamoja na hatua

nyingine za uchaguzi. Jengeni utamaduni wa kukutana na wadau wenu wakati wa utekelezaji wa hatua mbalimbali za uchaguzi.

Nina imani ushirikiano huu utaendelea katika hatua zinazofuata ikiwemo kuwahamasisha na kuelimisha wananchi waliojiandikisha kujitokeza kwa wingi **tarehe 27 Novemba, 202**4 siku ya kupiga kura. Nitoe wito kwa wadau wote kuwa nguvu na mikakati iliyotumika katika uandikishaji iendelee kutumika kuelekea siku ya kupiga kura ya tarehe 27 Novemba, 2024 ili wananchi wote waliojiandikisha wajitokeze kupiga kura kuwachagua viongozi wanaowataka.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

**Mhe. Mohamed Mchengerwa (MB)**
**Waziri wa Nchi, OR – TAMISEMI**

**21.10.2024**